

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA FEDHA NA UCHUMI



TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

SERIKALI YATENGA SHILINGI 20 BILIONI KWA AJILI YA KUTOA MIKOPO YA KILIMO

“Katika kutekeleza Sera ya kuwawezesha wananchi kiuchumi Serikali imetenga kiasi cha shilingi 20 bilioni katika mwaka wa fedha wa 2009/10. Fedha hizo zitatolewa na benki ya rasilimali kwa kuwakopesha wakulima”. Alisema Mhe. Omari Y. Mzee (Mb) kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, wakati akijibu swali la Mhe. Mbarouk K. Mwandoro (Mb), Mkinga, bungeni leo.

Mhe. Mzee alieleza kuwa, Juhudi za kuzishawishi Benki za biashara ili kuzikubali hati miliki za ardhi za kimila kama dhamana ya mikopo zinaendelea vizuri na tayari benki ya CRDB imeanza kutoa mikopo kwa kutumia hati hizo. Kulingana na kanuni za benki za biashara zinazotoa mikopo, dhamana ya mikopo ni moja ya kigezo kinachohitajika kabla ya kupatiwa mikopo. Vigezo vingine ambavyo ni muhimu ni pamoja na mchanganuo wa biashara, uwezo wa mkopaji wa kulipa deni analotaka kukopa, uwezo wa mkopaji wa kuendesha biashara, historia ya mkopaji ya kuweka fedha benki pamoja na mwenendo wake wa kulipa madeni.

“Ili fedha hizo ziwafikie wakulima wengi zaidi na hasa wale wadogo walioko vijijini, benki ya rasilimali itakopesha fedha kupitia SACCOSS, VICOBA, Vyama vya Ushirika, Benki za Jamii na Vyama vya Wakulima wa nje (Outgrowers Associations). Benki ya rasilimali imejiandaa kufungua ofisi za kanda ili kutoa huduma karibu zaidi na wakulima. Benki ya rasilimali itatumia wakala wa usambazaji wa zana za kilimo. Wakala hao watatoa pia mafunzo kwa wakulima pamoja na kupewa jukumu la kufanyia matengenezo vifaa vya kilimo vya wakulima”. Alifafanua Mhe. Mzee.

Mhe. Mzee ameeleza kuwa Serikali itatoa fedha kwa benki ya rasilimali ili ukopeshwaji wake uwe wa riba nafuu ambayo ni kati ya asilimia 5 hadi 8 kwa mwaka. Mikopo itakayotolewa italipwa kwa kipindi cha kati ya miezi sita hadi miaka 15, kuendana na mahitaji ya mradi. Marejesho ya mikopo yatafangwa kuendana na msimu wa kilimo. Dhamana itahusisha mali ambazo wananchi wa vijijini wanazo kama vile ardhi na mashine.

“Wakulima kabla ya kupatiwa mikopo watasaidiwa kuandaa michanganuo ya biashara. Barabara zinazokwenda mashambani zitaboreshwa ili mazao ya mkulima yaweze kufika sokoni kwa urahisi, kufanya hivyo kutasaidia kumpatia mkulima mapato mengi zaidi. Kupanua miundombinu ya umwagiliaji ili kuongeza uzalishaji” ameingiza Mhe. Mzee.

Bunge linaendelea na Mkutano wa Kumi na Nane kwa majadiliano ya Kikao cha kumi na mbili.

IMETOLEWA NA MSEMAJI MKUU

WIZARA YA FEDHA NA UCHUMI

DODOMA

09/02/2010